# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS
TANZANIA

Toleo la 85
Julai - Agosti 2019

## MAKAMU WA RAIS AZINDUA PROGRAMU YA KUHAMASISHA USALAMA WA WANAWAKE NA WASICHANA




Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan akibeba ishara inayotoa wito wa kukomeshwa kwa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake katika maeneo ya masokoni wakati wa uzinduzi wa programu hiyo jijini Dodoma, Julai 30, 2019. **Picha | Chama cha Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT)**

Makamu wa Rais atoa wito kwa Watanzania kusimama imara na kupinga vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia pahali pa kazi. Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa wananchi wote kutimiza wajibu wao katika kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika maeneo yote. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa progamu mpya inayolenga kuimarisha usalama wa wanawake na wasichana katika maeneo ya masokoni katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga,

***Inaendelea Ukurasa wa pili (2)***

## VIDOKEZO

- Mpango atoa taarifa mpya kuhusu utekelezaji wa SDGs
- Siku ya Kukumbukwa ya Nelson Mandela kwa Wanafunzi Wanaotatua Matatizo ya Wanaotumia Dawa za Kulevya
- Jengo la Umoja wa Mataifa Tanzania laanza kutumia nishati ya jua
- Umoja wa Mataifa wasisitiza umuhimu wa kuwasaidia wakulima wa mwani wanawake

## Kauli ya Serikali

***“Ninafurahi kuona kuwa sekta binafsi imewakilishwa hapa. Tunatumaini kwamba uwezo wao wa kifedha na kiufundi utatumika katika kufikia malengo haya. Ninafurahi pia kuona vyama vya kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali yameungana nasi ili kuona kwamba ripoti ambayo sote tulishrikiana kuiandaa inawasilishwa Umoja wa Mataifa. Vilevile, ninafurahi kuona kwamba Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez, ameungana na ujumbe wetu ili kuwawakilisha washirika wengine wa maendeleo wanaotuunga mkono katika utekelezaji wa SDGs.”***

**Waziri wa Fedha na Mipango , Mh. Dkt. Philip Mpango Akitoa shukrani zake kwa wadau wote kwa kushiriki kwao katika mchakato wa VNR Julai, 2019**

*Kutoka ukurasa wa Kwanza (1)*



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan akizindua programu ya UN Women na Serikali yenye lengo la kuhakikisha usalama wa wanawake na wasichana katika maeneo ya sokoni katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Hlamashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Programu inafadhiliwa na Serikali ya Sweden. **Picha | Chama cha Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT)**

*"Hili ni suala linalotugusa sisi sote. Sote tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba wanawake na wasichana, na jamii zetu zinaishi kwa amani,"*

**Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais**

Makamu wa Rais alisema vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia vinaendelea kuleta matatizo mengi katika jamii kote nchini, ambapo aliongeza kusema kwamba kila mmoja ana wajibu wa kuchukua hatua na kupinga vitendo hivyo.

"Hili ni suala linalotugusa sisi sote. Sote tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba wanawake na wasichana, na jamii zetu zinaishi kwa amani," alisema.

Jihihada hii mpya inatokana na ushirikiano kati ya UN WOMEN na Chama cha Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT), kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden. Jitihada hiyo italenga kujenga ushirika unaohusisha sekta mbalimbali, kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa kukuza ukusanyaji data ili kuwaruhusu wanawake wafanyabiashara masokoni kufanya bishara katika mazingira salama.

Akizungumza katika tukio hilo, Mwakilishi wa UN WOMEN, Bi. Hodan Addou, alisema mamlaka za serikali za mitaa zina nafasi muhimu katika kuhakikisha kwamba maeneo ya sokoni panakuwa salama kwa wanawake na wasichana. "Kupitia kuimarishwa kwa sheria ndogondogo za halmashauri na kushirikiana na wadau, kwa pamoja tunaweza kufanya maeneo ya sokoni kuwa salama zaidi. Mradi huu wa majaribio, kwa hiyo, ni muhimu sana ili kupata mfano mzuri wa njia bora za kufanya ambazo halmashauri nyingine zinapaswa kuiga ili kuleta matokeo bora kote nchini," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mratibu na Mkurugenzi wa Nchi wa UNAIDS, Dkt. Leopold Zekeng Achengui, alisisitiza wajibu muhimu wa mamlaka za serikali za mitaa katika kuhakikisha kwamba haki za wanawake zinazingatiwa katika maeneo ya sokoni na ya umma. "Programu zinazotekelezwa na halmashauri zinapaswa kuzingatia masuala ya jinsia, zitokane na utafiti, na ziendane na maeneo yenyewe. Kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika maeneo ya sokoni kunahitaji wadau wengine ambao wako karibu zaidi ya jamii zinazohusika.

*Inaendelea Ukurasa wa tatu (3)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa pili (2)*

Halmashauri ndiyo hasa zinazoendana na hitaji hilo," alisema.

Zaidi ya hayo, Dkt. Achengui alieleza kwamba programu hiyo itaendelea kusaidia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Kukomesha Vitendo vya Ukatili Dhidiya Wanawake na Watoto ambao unalenga kupunguza matukio ya ukatili walau kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022, kuchangia ufikiwaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, lengo la 5 linalohusu Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake.

## UMOJA WA MATAIFA WASISITIZA UMUHIMU WA KUWASAIDIA WAKULIMA WA MWANI WANAWAKE




Wadau wa Mnyororo wa Thamani katika Zao la Mwani wakiandamana kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mwani Kitaifa. Tasnia ya kilimo cha mwani ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi kwa Zanzibar nyuma ya utalii na kilimo cha karafuu, na inaajiri zaidi ya watu 24,000, ambapo miongoni mwao asilimia 80 ni wanawake. **Picha | Agnes Kenneth/ UN Tanzania.**

Siku ya Kitaifa ya Mwani iliadhimishwa mwishoni mwa mwezi Julai kwa lengo la kukuza welewa kuhusu kilimo cha mwani, uchakataji na matumizi yakiwemo manufaa ya kiafya ya bidhaa zake. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa: "Mwani kwa Afya Yako". Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Klasta ya Walima Mwani Zanzibar kwa kushirikiana na Taasisi ya Milele ya Zanzibar na COSTECH. Wadau wengine walioshiriki ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) na Mamlaka ya Biashara ya Tanzania (TanTrade).

Tasnia ya mwani ni miongoni mwa sekta kubwa za kiuchumi Zanzibar nyuma ya utalii na kilimo cha karafuu. Tasnia inaajiri wakulima 24,000, ambapo asilimia 80 yao ni wanawake. Changamoto kubwa wanayokabiliana nayo wanawake wajasiriamali ni upatikanaji wa mtaji ili kukuza biashara zao, bei ndogo ya mwani na kutegemea vifaa duni katika kufanya kilimo cha mwani.

*Inaendelea Ukurasa wa nne (4)*

*Kutoka ukurasa wa tatu (3)*

Aliyekuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Hassan Khamis Hafidh, alisema kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imedhamiria kuwekeza katika kilimo na uchakataji wa mwani. Alisema kuwa kwa wastani, kilimo cha mwani kinazalisha Shilingi bilioni 3 kwa mwaka, akiongeza kwamba kiasi hiki kingeweza kuongezeka sana kama kungekuwa na uongezaji thamani hapahapa nchini. Vilevile alisema kwamba SMZ imewaalika wawekezaji kutoka Indonesia ili kuanzisha kiwanda cha uchakataji mwani huko Pemba, akisisitiza kwamba jitihada hizo zitasaidia kupandisha bei ya shambani ya mwani hadi zaidi ya Shilingi 3,000 kwa kilo.

Mratibu wa shughuli za Umoja wa Mataifa katika Eneo la Zanzibar, Bi. Dorothy Temu-Usiri, alizungumzia mchango wa Umoja wa Mataifa kupitia Mpango wa Pamoja wa Zanzibar (ZJP) ambapo moja ya maeneo inayoshughulikia ni 'Kuwawezesha wanawake kupitia Ukuzaji wa Mnyororo wa Thamani wa Zao la Mwani'. Eneo hilo la ZJP linasimamiwa na FAO na kuhusisha UNIDO, UN WOMEN (ambapo mashirika haya yanakazia masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani) na vilevile Shirika la Kazi Duniani (ILO) (ambalo linakazia ajira zenye hadhi na masuala ya ajira ya watoto katika tasnia ya kilimo cha mwani). Lengo kuu ni kuwa na nguvu ya pamoja miongoni mwa mashirika ili kufikia malengo yanayofanana, kwa nia ya kuimarisha ustawi wa maisha ya wakulima wa mwani huko Zanzibar.

Kwa upande wao, msemaji wa FAO, Ali Haji Ramadhani, alisema kwamba shirika lake linaendelea kuunga mkono uzalishaji wa mwani na ukuzaji wake, huku Ofisa wa Programu wa Taifa wa UNIDO, Gerald Runyoro, akizungumzia msaada wa kiufundi ambao UNIDO inatoa ili kuimarisha uongezaji thamani katika zao na kuimarisha masoko.



Vijana wakiwa katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Vijana ambayo yalifanyika mkoani Dodoma. Maofisa wa Serikali na Umoja wa Mataifa walizungumzia umuhimu wa vijana kutimiza wajibu wao katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu. **Picha | Warren Bright UNFPA**



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

## KUWAPA VIJANA NAFASI YA KWANZA




Katika hotuba yake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mh. Selemani Said Jafo, akisisitiza kwamba mashirika yasiyo ya Kiserikali, hasa nchini Tanzania, yamesaidia kuwaunganisha vijana na kuwaleta pamoja. **Picha | Warren Bright UNFPA**

Zaidi ya vijana 600 kutoka kote nchini Tanzania walikutana jijini Dodoma ili kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana. Ujumbe mkuu ulikuwa: "Kuelekea 2030 na Tanzania ya Viwanda: Kuimarisha Elimu ya Vijana kwa Maendeleo ya Taifa". Maadhimisho hayo yaliandaliwa na serikali, UNFPA, ILO, UNICEF na UNESCO, kwa uungaji mkono wa washirika wa Umoja wa Mataifa na mashirika ya hapa nchini na ya kimataifa yasiyo ya kiserikali. Mgeni rasmi alikuwa Mh. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mwakilishi wa UNFPA, Bi. Jacqueline Mahon; Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Vijana ya Zanzibar, Bw. Amour Hamid Bakari, na mamlaka za mitaa nao pia walihudhuria. Tukio hilo lilitoa fursa kwa vijana kuzungumza kwa kauli moja, kushirikishana uzoefu kuhusu elimu jumuishi na, kwa upana zaidi, matarajio yao kuelekea Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu. Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) nchini Tanzania hapo ifikapo mwaka 2030 hakutawezekana bila ushiriki kamili na wenye ufanisi wa vijana. Elimu kamili, inayofaa na inaotolewa kwa usawa ile inayofundisha zaidi ya mambo ya darasani inapaswa kukidhi mahitaji na matakwa ya sasa ya vijana wa Tanzania,

*"Kuelekea 2030 na Tanzania ya Viwanda: Kuimarisha Elimu ya Vijana kwa Maendeleo ya Taifa"*

*Inaendelea Ukurasa wa sita (6)*

*Kutoka ukurasa wa tano (5)*

wakiwemo wale walio katika makundi ya wanyonge. Mkurugenzi Mtendaji wa Peace Life for People with Disability Foundation, Bi. Sophia Mbeyela, alitoa hotuba iliyosisimua akizungumzia changamoto ambazo vijana wenye ulemavu wanakabiliana nazo katika kupata elimu, ikiwemo elimu ya ngono na afya ya uzazi. Alisisitiza kwamba, ili elimu iwe jumuishi, haina budi kuheshimu uwezo na kuakisi na kuendana na hali halisi na utambulisho wa watu wa kundi hilo.

Mgeni Rasmi, Mh. Selemani Jafo, alisisitiza juu ya nguvu ya vijana katika kusukuma maendeleo yao huku akirejea ahadi ya serikali ya kuwasaidia ili wazitumie fursa vizuri. Akizungumza kwa niaba ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa nchini, Bi. Mahon, alirejea kauli zinazosema kwamba vijana ni washiriki motomoto wa ujumuishi na kupatikana kwa elimu na pia kama wasukuma mabadiliko, wavumbuzi na wajasiriamali ambao wanaweza kuleta masuluhisho bora na yaliyo jumuishi zaidi na yanayosaidia kukabiliana na changamoto wanazokabiliana katika hali halisi.

Tukio hilo pia lilikuwa fursa kwa vijana kujadiliana kuhusu ujumbe wanaotaka kuufikisha katika Mkutano Mkuu wa Nairobi hapo Novemba 12 hadi 14, mwaka huu ili kuweka juhudi za pamoja kumalizia kazi iliyokuwa haijamalizika ya Kongamano la Kimataifa la Idadi ya Watu na Programu ya Maendeleo ya Utendaji, na hivyo kutimiza ahadi iliyotolea kwa vijana miaka 25 iliyopita ya kuunda Tanzania ambapo kila kijana bila kujaali anaishi wapi anaweza kufanya uamuzi wake mwenyewe na kutumai haki zake za afya ya uzazi.



Vijana wakiwa katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Vijana ambayo yalifanyika mkoani Dodoma. Maofisa wa Serikali na Umoja wa Mataifa walizungumzia umuhimu wa vijana kutimiza wajibu wao katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu. ***Picha | Warren Bright UNFPA***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# RIPOTI MAALUMU
# MPANGO ATOA TAARIFA MPYA KUHUSU UTEKELEZAJI WA SDGS



Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez, akipeana mkono na Waziri wa Fedha na Mipango, Mh. Dkt. Philip Mpango, akimpongeza baada ya Tanzania kuwasilisha ripoti yake ya Mapitio ya Kitaifa ya Hiyari kuhusu Utekelezaji wa SDGs. **Picha | UN Tanzania**

Mwezi Julai, 2019, Mh. Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango aliongoza ujumbe wa Tanzania katika Jukwaa la Viongozi wa Ngazi ya Juu wa Kisiasa (High-Level Political Forum (HLPF)) lililojadili Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) huko jijini New York. Katika jukwaa hilo, Tanzania iliwasilisha ripoti yake ya kwanza ya Mapitio ya Hiyari ya Kitaifa (VNR) kuhusu utekelezaji wa SDGs, ambapo ilionyesha hatua za utekelezaji huo kwa upande wa serikali na wadau wasio wa serikali, yote yakifanyika kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa na wadau wengine. Mratibu Mkazi wa UN, Bw. Alvaro Rodriguez, aliuwakilisha Umoja wa Mataifa Tanzania katika Jukwaa hilo.

Ripoti ya Tanzania katika Jukwaa la HLPF, ambayo ilifafanuliwa vizuri na Waziri Mpango, ilipokelewa vizuri na wanajukwaa kwani ilionyesha kwamba kuna ukuaji chanya wa uchumi na kuendelea kupungua kwa umaskini (ingawa si kwa kiwango cha juu kama ilivyokuwa imetarajiwa); kuimarika kwa elimu na afya; kuimarika kwa taasisi; utawala bora; kuimarika kwa ujumuishwaji wa kifedha; kinga ya jamii na mapambano dhidi ya ufisadi.

Changamoto za kufikia SDGs ambazo Waziri Mpango alizianisha ni pamoja na uingizwaji/usafirishaji wa fedha haramu (IFF); kukosekana kwa rasilimali pesa, uwezo na teknolojia ya kusaidia SDGs; na changamoto za kimazingira zinazotishia uhai katika mazingira na majini. Dkt Mpango alitoa wito kwa washirika kuunga mkono juhudi za Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo.

Akitoa shukrani zake kwa wadau wote kwa kushiriki kwao katika mchakato wa VNR, Waziri Mpango alisema: “Ninafurahi kuona kuwa sekta binafsi imewakilishwa hapa. Tunatumaini kwamba uwezo wao wa kifedha na kiufundi utatumika katika kufikia malengo haya.

*Inaendelea Ukurasa wa nane (8)*

*Kutoka ukurasa wa saba (7)*



Mratibu wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez, akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango, Mh. Dkt. Philip Mpango, na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, jijini New York, Balozi Modest Mero (katikati) wakishangilia kwa pamoja baada ya ripoti ya Tanzania ya VNR kupokelewa vema katika Jukwaa la HLPF kuhusu masuala ya SDGs. **Picha | UN Tanzania**

Ninafurahi pia kuona vyama vya kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali yameungana nasi ili kuona kwamba ripoti ambayo sote tulishrikiana kuiandaa inawasilishwa Umoja wa Mataifa. Vilevile, ninafurahi kuona kwamba Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez, ameungana na ujumbe wetu ili kuwawakilisha washirika wengine wa maendeleo wanaotuunga mkono katika utekelezaji wa SDGs."

Kwa upande wake, Bw. Rodriguez alisisitiza kwamba: "Tumeshuhudia upigwaji mzuri wa hatua na serikali inafanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba kila msichana na mvulana anapata elimu bora na matunzo bora ya afya. Pia kuna juhudi za kutosha za kulinda mazingira, kukabiliana na changamoto za ukosefu wa ajira na pia kupiga vita tofauti kati ya wanaume na wanawake." Hata hivyo, alisema kwamba: "Bado kuna changamoto nyingi. Yatupasa kushughulikia tatizo la fedha haramu ambapo rasilimali za Afrika, Tanzania na nchi nyingine zinaporwa badala ya kuwekezwa katika bara hilo ili kuendeleza vipawa vya Watanzania akina baba, akina mama, wavulana na wasichana.

Tathmini ya haraka ya VNRs inaonyesha kwamba, nchi nyingi zinazoendelea zinapambana kufikia malengo ya SDGs kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali fedha ili kuteleza malengo yanayohusika. Taarifa ya fedha ya UNDESA kwa Jukwaa la HLPF ilionyesha mwenendo wa kushuka kwa Misaada Rasmi ya Maendeleo (ODA) kwenda katika nchi zinazoendela. Nchi hizi zinatarajiwa kutafuta fedha na kutumia rasilimali zake ili kutekeleza Malengo ya SDGs.

Mapendekezo ya jumla kutoka katika Jukwaa ambayo yanaihusu Tanzania katika kufikia SDGs ni pamoja na: kuimarisha ushirikishwaji wa wadau wengi zaidi ili kukomesha fedha haramu; kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika SDGs, kupunguza ukosefu wa fedha; kushughulikia migogoro na matumizi ya nguvu ili kujenga uchumi unaoongozwa na usalama wa watu.

*Inaendelea Ukurasa wa tisa (9)*



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa nane (8)*

Mafunzo yanayotokana na yaliyojadiliwa katika Jukwaa la HLPF yanatia moyo kwamba serikali inafanya kazi kuhakikisha kwamba utekelezaji wa SDGs unafanikiwa kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa na wadau wengine. Suala hili hatimaye litaiweka Tanzania katika njia sahihi ya kufikia Dira yake ya Maendeleo ya 2025 na Malengo ya SDGs ifikapo mwaka 2030.




Mratibu wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez, akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango, Mh. Dkt. Philip Mpango (wa 5 kulia), Mh. Fatma Hassan Toufik (MB), Viti Maalumu (wa 4 kulia), Dkt. Lorah Madete, Mratibu wa SDGs, Wizara ya Fedha na Mipango (wa 3 kulia) na Bi. Ngusekela Nyerere, Mchumi, Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (wa 1 kushoto) wakati wa mkutano wa Jukwaa la HLPF katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York. **Picha | UN Tanzania**



Mratibu wa Umoja wa Mataifa, Bw. Alvaro Rodriguez, akiwa katika picha ya pamoja na Bw. Deus Kaganda, Kaimu Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Pande Nyingi, Wizara ya Mambo ya Nje a Ushirikiano wa Afrika Mashariki (wa 1 kushoto), Bw. Songelael Shilla, Msaidizi wa Balozi katika Ubalozi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, Jijini New York (wa 1 kulia), Bi. Ramla Khamis, Katibu wa Mabalozi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (katikati) na Bi. Ngusekela Nyerere (wa 2 kushoto), Mchumi, Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Matiafa, wakati wa mjadala wa Jukwaa la HLPF kuhusu SDGs. **Picha | UN Tanzania**

## FERRY ACROSS LAKE VICTORIA

Tarehe 29 Julai, kivuko MV Umoja Kilianza safari yake kupitia Ziwa Victoria uku kimebeba tani 720 za misaada ya kibinadamu ya chakula kwa ajili ya shughuli za WFP nchini Uganda na Sudan Kusini. Chakula kilisafirishwa kwenda Mwanza kwa reli na kisha mabehewa yalipandishwa moja kwa moja kwenye kivuko.

Hii ilikuwa ni safari ya 44 kwa kivuko kusafirisha chakula cha WFP katika ziwa, tangu shirika liunge mkono Serikali kufungua upya ukanda wa reli-ziwa-reli, Julai 2018. Njia hii haikuwa ikitumika kwa Zaidi ya miaka 10.


Tangu njia ilipofunguliwa, kivuko kimekuwa kikifanya kazi kusafirisha chakula sio tu kwa ajili ya WFP, ila pia bidhaa kwa ajili ya sekta binafsi. Njia hii inapunguza muda wa usafirishaji kwa asilimia 50 na ina kupunguza bei za usafirishaji kwa kiwango kikubwa.

Kufungua tena ukanda huu, WFP ilifanya kazi kwa karibu na Shirika la Reli Tanzania (TRC), Marine Services Company Limited Marine Services, Waratibu wa bandari Tanzania (TPA) na Shirika la Reli Uganda (URC).

Kama shirika ongozi la ugavi la Umoja wa Mataifa, WFP imeanzisha maeneo imara ya ugavi kwenye jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine sita ya kimkakati Tanzania. Maeneo ya ugavi ya WFP yaliopo Isaka na Dodoma hutumika kutoa misaada ya dharura katika nchi jirani.

Misaada ya kibinadamu inayopitia Tanzania huboresha sekta ya usafirishaji na kusaidia kukuza Tanzania kama mshindani wa ukanda wa usafirishaji. Asilimia arobaini ya hii ilitoka kwenye manunuzi ya ndani, zaidi kuimarisha uchumi na kusaidia wakulima wadogo.

Mwaka 2018, WFP iliingiza Dolla milioni 60 za Marekani katika uchumi wa ndani kwa manunuzi na ugavi huduma kwa kutumia ukanda wa Tanzania.






Wadau wa usafirishaji wa WFP na Serikali wakianza safari kutoka Bandari ya Kusini Mwanza itakayochukua saa 21 kuvuka Ziwa Viktoria hadi Bandari ya Bell nchini Uganda. Feri hiyo imebeba chakula cha msaada wa kibinadamu kwa ajili ya wakimbizi katika ukanda huu. **Picha | WFP/*Alice Maro***


This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# JENGO LA UMOJA WA MATAIFA TANZANIA LAANZA KUTUMIA NISHATI YA JUA



Hizi ni baadhi ya paneli za mfumo wa kisasa kabisa wa umeme wa jua ambazo zimefungwa katika Jengo la Umoja wa Mataifa. Ufungaji wa paneli 696 za umeme wa jua utasaidia kuzalisha asilimia 70 ya mahitaji ya umeme katika jengo hilo wakati wa saa za kazi. **Picha | UNDP Tanzania**

Hivi karibuni, shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), limeshereheka kuanza kutumia nishati endelevu baada ya kufunga Mfumo Chotara wa Nishati ya Jua katika Jengo la Umoja wa Mataifa jijini Dar es Salaam. Mfano huu wa kuigwa katika matumizi ya nishati rafiki ni uthibitisho kwamba UNDP inaongoza kwa kuwa mfano katika kutekeleza jitihada ya kuleta Nishati Endelevu kwa Wote (SE4ALL) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Kaimu Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Bi. Verity Nyagah, alisema: "Kufunga kwa mafanikio Mfumo wa Kisasa wa Nishati ya Jua katika Jengo la Umoja wa Mataifa kunatoa mwongozo kwa mashirika mengine, ya umma na binafsi, kuiga mfano huu, ili kuisaidia nchi kutekeleza Jitihada za Umeme Endelevu kwa Wote (SE4ALL) na pia kutekeleza Mchango Uliodhamiriwa Kitaifa (NDC) wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania."

Hapo kabla, jengo hili lilikuwa likitumia umeme kutoka kwenye gridi ya taifa kwa kusaidiwa na genereta zinazotumia mafuta mengi ya dizeli, njia zote mbili zikiwa na gharama kubwa na zisizo za kutegemewa sana. Baada ya kuleta ufumbuzi wa nishati ya jua, asilimia 70 ya matumizi ya umeme katika jengo hili yatatokana na mfumo wa umeme wa jua usiotoa hewa ya ukaa. Kiwango cha hewa ya ukaa kitakachoepukwa kitaongeza ufanisi wa Jengo la Umoja wa Mataifa katika kupunguza hewa ukaa ambayo ni mzigo kwa mazingira. Hii inaendana na ufikiwaji wa Lengo la 13 la SDGs—Kuchukua Hatua Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi na hivyo kuhamasisha utekelezaji wa Lengo la 7—Kuanza kutumia Nishati Rafiki yenye Gharama Nafuu", yote haya yakiwezekana kwa ubunifu huu wa suluhisho la nishati rafiki, hatua ambayo itayapa mashirika mengine hamasa ya kuiga. Mfumo huo utaimarisha uwiano wa maisha binafsi na kazi,

*Inaendelea Ukurasa wa kumi na mbili (12)*

***Kutoka ukurasa wa kumi na moja (11)***



Ilikuwa na nderemo na vigelegele pale Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Hamis Mwinyimvua alipozindua rasmi mfumo wa umeme wa jua uliofungwa katika Jengo la Umoja wa Mataifa, jijini Dar es Salaama. **Picha | UNDP Tanzania**

kwani mfumo wa umeme wa jua hautoi kelele za aina yoyote ile, tofauti na jenereta zenye makelele na bughudha. Haya ni manufaa yanayopimika kwa upande wa UNDP na mashirika mengine na hata kwa taasisi za serikali zinazofanya kazi na UNDP, jambo linalodhihirisha umahriri wa UNDP wa kutekeleza yale inayoyahubiri—maendeleo endelevu ya watu.

Kwa upande wa gharama, mfumo wa nishati ya jua utaokoa takribani $34,618 kwa mwaka zilizotumika katika kulipia nishati (kwa kuondoa mfumo wa umeme wa gridi ya taifa na majenereta), na gharama iliyotumika kufunga mfumo huo itafutwa ndani ya kipindi cha miaka 12.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Hamis Mwinyimvua, ambaye alimwakilisha Waziri wa Nishati, Mh. Medard Kalemani (MB) alisema: “Uzuri wa teknolojia ya Nishati Mbadala ni kwamba inaweza pia kutekelezwa katika mifumo tofauti; baadhi wanaweza kutumia miundombinu iliyopo kama vile majengo, reli na vituo vya mabasi na hivyo kuepuka matumizi ya ardhi kubwa ambayo itatumika kwa matumizi mengine. Kupitia mfumo huu, UNDP imeonyesha uwezekano wa kutumia nafasi ya ofisi katika kuendeleza nishati endelevu.”




Katibu Mkuu katika Wizara ya Nishati, Dkt. Hamis Mwinyimvua, akizindua mfumo wa kisasa wa umeme wa jua akisaidiana Dancilla Mukarubayiza, ambaye ni Kaimu Mwakilishi wa zamani wa UNDP huku Mwakilishi wa Zamani wa UNDP Verity Nyagah akitazama. **Picha | UNDP Tanzania**



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# SIKU YA KUKUMBUKWA YA NELSON MANDELA KWA WANAFUNZI WANAOTATUA MATATIZO YA WANAOTUMIA DAWA ZA KULEVYA



Ofisa wa Kampuni ya Simba Cement akikabidhi mifuko ya saruji kwa walimu na mwenyekiti wa Shule ya Msingi Mchikichini. Saruji hiyo itatumika kufanya ukarabati wa uzio unaozunguka shule hiyo. **Picha | UNIC/*Laurean Kiiza***

*"Chukua hatua, hamasisha mabadiliko, na ondoa umaskini"*

Mwaka huu ni kumbukumbu za miaka 10 tangu Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa litangaze Siku ya Kimataifa ya Nelson Mandela. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa: "Chukua hatua, hamasisha mabadiliko, na ondoa umaskini". Maadhimisho ya kitaifa yalifanyika katika Shule ya Msingi Mchikichini, ambayo inakabiliwa na tatizo la kukosa uzio jambo ambalo limewapa nafasi vijana wanaotumia dawa za kulevya kuwaathiri wanafunzi na kutumia majengo kufanya uhalifu wao huo. Akizungumza katika maadhimisho hayo, Naibu Balozi wa Afrika ya Kusini nchini Tanzania, Bw. Frans van Aardt, alisema: "Nelson Mandela alitumia miaka 67 ya maisha yake kupiga vita ukiukwaji wa haki za binadamu. Ni kwa msingi huu kwamba watu kote duniani hutumia dakika 67 wakijitolea kuleta mchango chanya katika maisha ya watu wengine, iwe kwa namna ndogo au kubwa." Tamko la Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres kwa ajili ya siku hii lililosomwa na Ofisa Habari wa Umoja wa Mataifa Tanzania, Bi. Stella Vuzo. "Wito wa Nelson Mandela wa kujenga mshikamano katika jamii na kukomesha ubaguzi wa rangi bado unaendelea kuwa na maana hata leo, kwani kauli za chuki zinaendelea kutolewa hata sasa pahali mbalimbali ulimwenguni. Tunaposhirikiana ili kujenga amani, utulivu, kuleta maendelea endelevu na kutafuta haki ya kila mmoja, tutakuwa katika nafasi nzuri kwa kukumbuka mfano uliowekwa na Nelson Mandela," Bi. Vuzo alisoma. Mkuu wa Shule ya Msingi Mchikichini, Bw. Wilson Mahemba, aliwafahamisha waliohudhuria tukio hilo kwamba watumia dawa za kulevya walikuwa tishio kubwa kwa wanafunzi shuleni hapo. "Mara nyingine watumiaji dawa za kulevya hawa hutupa ovyo katika mazingira ya shule sindano walizotumia kujidunga, na wanafunzi wadogo huziokota na kuzichezea, na mara nyingine wavulana hufundishwa kutumia dawa hizo na hivyo nao kuwa watumia dawa za kulevya," alieleza.

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na nne (14)***

*Kutoka ukurasa wa kumi na tatu (13)*

Bw. Mahemba alieleza pia kwamba viwango vya ufaulu vya wasichana katika shule hiyo daima huwa ni bora kuliko wavulana. Alisema hiyo ni kwa sababu ya athari za dawa za kulevya, "wavulana wanafanya vibaya katika masomo kwa sababu wanatumiwa kusambaza dawa za kulevya na baadhi yao tayari ni watumiaji wa dawa hizo."



Wageni, wanafunzi wa Shule ya Msingi Mchikichini, walimu na vijana wakifuatilia wakati Klabu ya Mazingira ya Shule ya Msingi Mchikichni walipotumbuiza katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Nelson Mandela. **Picha |UNIC/ *Harriet Macha***

Maadhimisho hayo pia yaliendana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na pia Mkakati mpya wa Serikali ya Afrika ya Kusini wa kuchukua hatua madhubuti zaidi katika kuleta ufumbuzi ili kweli kupata matokeo endelevu. Katika mkakati huu mpya katika Siku ya Nelson Mandela, maeneo muhimu yaliyobainishwa ili kupewa kipaumbele katika ushirikiano wa kimataifa ni pamoja na elimu na kueneza usomaji, chakula na lishe, makazi, usafi wa mazingira na uraia wenye uwajibikaji.

Tukio hilo lilihudhuriwa na Jamii ya Wanadiplomasia, raia wa Afrika ya Kusini waishio nje ya nchi yao, watendaji na wadau wa makampuni na taasisi za kutoka Afrika Kusini kama vile Simba Cement, Nabaki Afrika, Coca Cola, Pepsi, Stanbic, FNB, Spik and Span, Nipe Fagio, Vijana kutoka Mtandao wa Maendeleo ya Vijana wa Temeke na wanakikundi cha mazoezi yam bio cha Wakali.



Bw. Godfrey Ten, anayetoka katika Mtandao wa Maendeleo ya Vijana wa Temeke, akizungumza na vijana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Nelson Mandela na mpango wa elimu mitaani kwa ajili ya vijana wenye matatizo ya kutumia dawa za kulevya. **Picha | UNIC/*Laurean Kiiza***



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

# WAATHIRIKA SI WAHALIFU, WALINDE




Mkuu wa IOM akizungumza na washiriki wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu. **Picha | IOM**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Wahamiaji (IOM) kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani wameadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupinga Usafirishaji Binadamu mwishoni mwa mwezi Julai katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Tukio hilo lilitanguliwana Mjadala wa Kitaifa uliofanyika siku moja kabla.

Kama sehemu ya Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II), IOM ndio shirika linaloongoza kwa kufanya kazi kwa karibu na serikali katika kuzuia na kukabiliana na Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu (TIP). Kwa mujibu wa IOM, biashara hii ni ukiukwaji wa kiwango cha juu cha haki za binadamu. Kwa hiyo, ni muhimu kuendelea kuchukua hatua za dhati kukomesha biashara hii haramu, ambapo ujumbe katika maadhimisho ya mwaka huu ulikuwa: “Isaidie Serikali Kukomesha Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu; Waathirika Si Wahalifu, Walinde”.

Sambamba na juhudi za kuimarisha uwezo wa wadau wakuu katika kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji wanawake na watoto, IOM ilikutana na viongozi wa dini 247 na viongozi wa mitaa, na wanajamii 148 kupitia vipindi vya mazungumzo ya kijamii katika mwaka uliopita. Hatua hii imesaidia kuleta ushiriki mkubwa zaidi wa viongozi hawa katika kuiunga mkono IOM na Serikali ili kuzuia na kuchukua hatua dhidi ya biashara hii haramu katika maeneo yao.

> *“Isaidie Serikali Kukomesha Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu; Waathirika Si Wahalifu, Walinde”*

***Inaendelea Ukurasa wa kumi na sita (16)***

***Kutoka ukurasa wa kumi na tano (15)***

Hatua hii imesaidia kuleta ushiriki mkubwa zaidi wa viongozi hawa katika kuiunga mkono IOM na Serikali ili kuzuia na kuchukua hatua dhidi ya biashara hii haramu katika maeneo yao. Zaidi ya hayo, kujenga uwezo wa watendaji walio mstari wa mbele kumesaidia kuimarisha ushirikiano mongoni mwao katika kukabiliana na matukio ya biashara haramu ya binadamu.

Katika kuadhimisha siku hiyo, IOM inashirikiana na wadau ili kuhakikisha kwamba mifumo ya msaada na kinga kwa waathirika inafanya kazi sawasawa. Mpango madhubuti wa kuimarisha juhudi na kukabiliana na biashara haramu ya binadamu nchini Tanzania ulianzishwa wakati wa Majadiliano ya Kitaifa.

Wakati wa maadhimisho hayo, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. Kangi Lugola, aliwatunuku IOM cheti cha utambuzi kwa mchango wake mkubwa katika kukomesha tatizo la biashara haramu ya usafirishaji binadamu. Mkuu wa IOM, Dkt. Qasim Sufi, alimshukuru Waziri kwa utambuzi huo na kurejea ahadi kwamba "IOM itaendelea kuwa tayari kuchukua hatua madhubuti zinazolenga kuongeza kasi ya kiutawala na taratibu za kisheria ili kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu."

*"IOM itaendelea kuwa tayari kuchukua hatua madhubuti zinazolenga kuongeza kasi ya kiutawala na taratibu za kisheria ili kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu."*

**Dr. Qasim Sufi,**
**Mkuu wa IOM**

IOM ilitambua msaada inaoupata kutoka katika serikali za Ufalme wa Sweden, kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA), na Serikali ya Norway, kwani misaada hiyo ina mchango mkubwa katika kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu nchini Tanzania.




Maofisa wa ubalozi kutoka Burundi, Ethiopia, Korea Kusini, na Norway wakitembelea banda la Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM) wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu. **Picha | IOM**



This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021

## MATUKIO YAJAYO YA SIKU ZA KIMATAIFA

**September 21 -** Siku ya Kimataifa ya Amani

**October 11 -** Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike

**October 16** - Siku ya Chakula Duniani

**October 24 -** Siku ya Umoja wa Mataifa

**November 19 -** Siku ya Choo Duniani

## UMOJA WA MATAIFA MADHUBUTI KWA DUNIA BORA ZAIDI

UNITED NATIONS
TANZANIA

**Ofisi ya Mratibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa**

+255 22 219 5021

info.untz@one.un.org

www.tz.one.un.org

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org. Website: www.tz.one.un.org Tel: (+255) 22-219-5021